

THAMANI YA KIFO CHA YESU KWAKO

Enzi za zamani, wanadamu walimwaga damu za wanyama kwaajili ya kuzifunika dhambi zao mbele za Mungu kama njia mojawapo ya upatanisho. Mungu akaona atoe kafara moja la thamani kuliko wanyama na chochote na kwa ajili ya watu woote, matajiri wenye wanyama wengi wa kutoa kafara hadi masikini ambao pengine walihangaika kutafuta mnyama wa kutoa kafara, kafara alilolitoa ni la Yesu Kristo.

Damu ya Yesu Kristo ilipomwagika, inao uwezo sio kufunika bali kufuta kabisa dhambi za mtu yeyote anayetubu nafasi ambayo ipo kwa watu wote wa dunia nzima, deni la damu lililipwa kwa watu woote. **Walawi 17:11, Ebrania 9:22**, pasipo kumwagika damu hakuna ondoleo la dhambi, na Damu ya Yesu ilikamilisha hitaji hilo kwetu.

KUMBUKA: Kila alichopitia Yesu katika maisha yake alipokuwa amevaa mwili wa nyama hapa duniani, kililenga kumkomboa mwanadamu katika maeneo mbalimbali ya maisha yake.

KUMBUKA: Wengi hawakumtarajia Yesu kuwa atakuwa masihi kulingana na walivyomwona, na yeye kuwa masihi kuliwastusha sana. Katika maisha, **HII INATUFUNZA KWAMBA** Mungu hachagui kama vile wanadamu wachaguavyo kwasababu yeye huangalia moyo na siku zote huwa anawashtusha sana wale wanaoangalia kwa jicho la kimwili. Hata katika maisha yako, ukiishi na Mungu vizuri hata kama wanadamu hawatakukudhania kufanya jambo fulani, Mungu huwa anawashangaza.

ISAYA 52:15 *ndivyo atakavyowasitusha mataifa mengi; wafalme watamfumbia vinywa vyao; maana mambo wasiyoambiwa watayaona; na mambo wasiyoyasikia watayafahamu.*

1) **HII NI KWASABABU WALIMDHARAU YESU.** Yesu alitokea kama surprise kwa wengi, na kwasababu alibeba kusudi la Mungu, alikutana na vipingamizi vyote vya shetani; alidharauliwa hadi mwisho ili sisi tusidharauliwe. **Isaya 53:3** *Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.*

- ✓ Yesu alipitia dharau na kukataliwa ili kwa kupitia yeye tusidharauliwe, tusiaibishwe wala tusiwe na roho ya kukataliwa. *(roho hizo hazina haki kukaa kwako kwani Yesu alishalipa garama yake, kama zipo zifukuze, zinatakiwa kuondoka).*
- ✓ Aliishi kama mche usio na nguvu (mwororo) na kama mzizi katika nchi kavu ili auchukue udhaifu wetu. Hakutoka familia yenye nguvu kipesa au kisiasa, alitoka familia isiyosifika kuwa na nguvu, ya selemera tu asiye na influence kisiasa au kiuchumi na hakuzaliwa ikulu. Cha kujifunza hapa ni kwamba,

1Korintho 1:27-29, Mungu huwa anatumia vitu unavyoona kama ni dhaifu na kuviinua mbele ya vile vinavyojiona vina nguvu; Yesu hakuwa tajiri, alitoka familia ya selemala tu, hakuwa na nyumba ndio maana alisema mbwena wana nyumba lakini yeye hana, na hata alipodaiwa kodi alimwamuru Petro akavue samaki afungue mdomo atakuta fedha atoe kodi. Hii haimaanishi wenye uwezo hawawezi kumbona Mungu, cha msingi ni kwamba, Mungu anahitaji moyo uliopondeka na kunyenyekea mbele zake, bila hivyo huwezi kumwona Mungu na hawezi kukutumia.

- ✓ **Yesu aliichukua roho ya kukataliwa ambayo wengi wanaishi nayo siku hizi.** Kuna watu hakuna chochote anakifanya kinaonekana ni kitu na watu wakiwaangalia wanaona hawana uwezo wa kufanya chochote na hawastahili chochote. Ukimwamini Yesu, atakusaidia kwa sababu yeye alipitia hiyo hali kwa ajili yetu na utakuwa huru.

Biblia inasema, alidharauliwa na kukataliwa na watu. Asingedharauliwa na kukataliwa asingekushinda kudharauliwa na kukataliwa; uzuri ni kwamba maisha hayo aliyaishi na kuyashinda kwa ajili yetu. Ukimtazama hakuwa na umbo wala uzuri, na watu walimhesabu sio kitu kabisa, kama vile watu wanavyoweza kukuhesabu wewe leo kuwa sio kitu, ila ukinwendea Yesu, atayatua mateso yako.

Isaya 53:1-3, *Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani? Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani. **Alidharauliwa na kukataliwa na watu**; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.*

- 2) **YESU ALIBEBA HUZUNI ZETU ZOTE.** Huzuni ni kinyume cha furaha na amani. Yesu ni mfalme wa amani, na amani yake haifanani na amani ambayo ulimwengu, pesa, ulinzi wa kidunia, cheo au chochote kinaweza kutoa na hilo lilikuwa moja wapo la lengo lake kuja duniani. **Isaya 53:3 anasema Yesu alikuwa mtu wa huzuni nyingi ajuaye sikitiko.** Wengi wana huzuni na masikitiko lakini hawajafikia kiwango alichokuwa amefikia Yesu, katika maisha yake alinyanyaswa hadi mwisho, lakini yote ili sisi tusinyanyaswe, ili sisi tuisikitike, ili sisi tuihuzunike. Ukiwa na masikitiko leo, mwambie Yesu, au yafukuze kwa Jina la Yesu, yanaondoka, na utakuwa na furaha na amani.

- ✓ **Isaya 9:6** Maana mtoto amezaliwa kwa ajili yetu, tumepewa mtoto wa kiume. Naye atapewa mamlaka kutawala. Ataitwa Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, **Mfalme wa Amani.** *(hapa haimaanishi tu kwamba ni mfalme ambaye hakuja na majeshi ya*

kimwili, ila pia anauwezo wa kuleta amani moyoni mwako kwasababu alihuzunika na kukosa amani badala yako).

- ✓ **Yohana 14:27** Yesu aliwaambia, Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo.
- ✓ **Wafilipi 4:7** Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zetu katika KRisto Yesu.
- ✓ **Yesu alihuzunika kiasi cha kutoa jasho la Damu.** Kisayansi, mtu akihuzunika hadi kufikia hatua ya mwisho, huwa anaweza kutoa jasho la damu au machozi ya damu; hili ni jambo halisi na sio kwamba lilitokea kwa Yesu kimiujiza, ni kwamba alihuzunika hadi kufikia hatua ya mwisho ambayo mwanadamu anaweza kuhusuzika.

Hii ndio hatua ya mwisho kabisa ya huzuni (**stress au depression**), na kisayansi inaitwa **hematohidrosis**, kitu ambacho ni nadra sana kutokea kwa mwanadamu na ni hatua ya mwisho kabisa ya huzuni. Pale Gethsemane Yesu alihuzunika kiasi kisichoelezeka, hadi akatoa jasho la damu. Kwa kuhuzunika huko, alibeba huzuni zetu zote na masikitiko yetu yote. Leo hii ukiona una huzuni au masikitiko, jua Yesu alishahuzunika badala yako hivyo ukimtwika yeue atakuweka huru na utakuwa na furaha na amani katika hali au mazingira yeyote unayoishi. **Luka 22:44 Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki, akazidi sana kuomba; hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchini.**

KUMBUKA; Kitu unachotakiwa kuelewa ni kwamba, Yesu hakuteswa au kuuawa kimiujiza. Aliteswa na kufanyiwa vyote hadi kifo kiuhalisia kabisa, alipata maumivu halisi, alihuzunika halisia ile kutoka jasho la damu sio kwamba lilikuwa jasho la kimiujiza ulikuwa uhalisia wa mwanadamu kama wewe kwamba ameumia moyo hadi kufika mwisho, alisikitika halisia na kuumizwa kiuhalisia na alikufa kihalisia kabisa. Ili kutukomboa wanadamu, alipovaa mwili wa mwanadamu alipitia shida zote ambazo mwanadamu angepitia ili azikomboe, na kwa njia hiyo tulikombolewa kikamilifu hakubakisha deni lolote kwenye huu mwili, roho na nafsi. Shetani hatudai kitu kabisa, Yesu alimaliza deni lote. Kama huzuni alishahuzunika kwa ajili yetu, kama maumivu aliyapata yote, kama kifo alikufa na kukishinda kwa kufufuka n.k hakuna alichobakisha. Hivyo unaposoma **Isaya 53** na injili jinsi Yesu alivyoteswa, usifikiri labda alifanya miujiza ya kujifanya anateseka wakati hateseni hapana, aliteseka kweli kiuhalisia kabisa kwa ajili yetu ndio maana thamani ya wokovu wetu haina kipimo kwasababu maumivu ambayo yalitupasa sisi yeye peke yake aliyabeba yote.

- ✓ **Isaya 53:4 Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu...**,

3) **DAMU YA YESU NI AGANO KATI YETU SISI NA MUNGU:** kama ilivyokuwa zamani kwamba watu wakitenda dhambi wanamwaga damu ya wanyama ili kufunika dhambi zao mbele za Mungu, Mungu alitoa kafara moja tu, la kifo cha Yesu, ili kupitia kifo cha Yesu Mungu atusamehe dhambi. Pasipo kumwamini Yesu huwezi kusamehewa dhambi, ila ukimwendea Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, lipo agano/mkataba kati yetu na Mungu na Mungu lazima atalitimiza, ataondoa dhambi zako na kukuweka huru.

- ✓ Agano la ondoleo la dhambi zetu. Bila Yesu, Mungu hakutambui. **Wakolosai 1:13,14** *“alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye (Kristo) tuna ukombozi, **Yaani msamaha wa dhambi**”*.

- ✓ **Agano na ushindi dhidi ya matunda yote ya dhambi.** Mshahara wa dhambi ni mauti, kufanya dhambi ni kufungua mlango mashetani yaingine kwenye himaya yako, na mwivi (shetani) haji ila kwa ajili ya kuua, kuchina na kuharibu. Mashetani yakija kwako, huja na magonjwa, laana, mikosi na yote mabaya, ndio maana kama vile ambavyo ungekimbia kifo kama kingekuwa kinaonekana kwa macho ndivyo unavyotakiwa kuikimbia dhambi kwasababu ikija kwako haiondoki bure, lazima ikuletee madhara.

Ni lazima tuishi kwa kujitambua kama askari vitani anavyokuwa macho muda wote kwasababu akizembea tu atampa adui nafasi ya kumdhuru. **1Petro 5:8** inasema *“**Mwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka zunguka, akitafuta mtu ammeze**”*.

Hata hivyo, matatizo yote aliyotuletea shetani maishani mwetu (magonja, n.k), Yesu aliyachukua yote pale msalabani. **Isaya 53:5**, *Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake **na kwa kupigwa kwake sisi tumepona***.

- ✓ **Damu ya Yesu inatusogeza karibu na Mungu: Waefeso 2:13** " *Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.*

Waebrania 10:19 " *Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu*

✓

4) **KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU NI USHINDI DHIDI YA SHETANI:** Yesu alipokufa alimshinda shetani na utawala wake wote. Baada tu ya kufufuka Yesu alisema katika **Mathayo 28:18, nimepewa mamlaka yote duniani na**

mbinguni. Shida zako zote, matatizo yako yote, yeyote au chochote duniani na mbinguni, viko chini ya mamlaka ya Yesu; kwa Jina lake vinatii.

- ✓ **Yohana 14:30** Mimi sitasema nanyi maneno mengi tena, kwa maana anakuja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu.
- ✓ **Ufunuo 1:18** Mimi ni Yeye aliye hai; nilikufa na tazama, mimi ni hai milele na milele! **Nami ninazo funguo za mauti na kuzimu.**
- ✓ **Wafilipi 2:10 -11** Ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani na vya chini ya nchi na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu KRisto ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.
- ✓ **Matendo 4:12** Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo kuokolewa kwalo.
- ✓ **Ufunuo 12:11;** *"Nao wakamshinda (shetani) kwa damu ya mwana-Kondoo na kwa neon la ushuhuda wao....(hata leo hii, yeyote aliye ndani ya Yesu, hadaiwi na shetani chochote kwasababu Yesu aliye ndani yake alilipa deni lote, hivyo ni suala la kumuamuru shetani kuondoka, kemea aondoke kwasababu hana haki kuishi ndani yako kwa namna yeyote ile. Kama wewe ni msafi na shetani hakudai chochote yaani dhambi, unayo mamlaka ya Jina la Yesu na shetani lazima atatii na kuondoka, ila kama anakudai, mfano, unamkemea wakati unatenda dhambi hauna Mungu moyoni, haondoki).*

- 5) **DAMU YA YESU INANENA MEMA JUU YA MAISHA YETU.** Damu huwa inaongea,tunakumbuka damu ya Habil ilinena, hivyo hata Damu ya Yesu inawez akunena mema, ikanena wokovu, ulinzi,uponyaji n.k katika maisha yetu kama tutakuwa tumempokea na kumwamini Yesu aliyeimwaga, naye ndiye njia pekee.

Waebrania 12;24 *"na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habil. "*

Kwa kifupi, yapo maandiko mengi yanayoonyesha uthamani wa Damu ya Yesu na kile inachoweza kufanya katika maisha yetu. Cha muhimu kukumbuka, tunaokolewa kwa njia ya kafara la Yesu Kristo, hakuna njia nyingine, tunaponywa kwa kafara lake kwasababu kwa kupigwa kwake tumepona, na tunafika mbinguni kwasababu yeye ndiye njia kweli na uzima. Ukimpokea Yesu na kuacha chambi/ukiwa ndani yake, unayo haki ya kudai haki zote ambazo Damu ya Yesu ilileta na unayo mamlaka ya kumwamuru shetani aondoke maishani mwako naye atatii kwasababu hana sababu ya kuwa kwako na lazima atii Jina la Yesu.

Hata hivyo, huwezi kumwamuru shetani kwa lolote kama hauna Mungu moyoni mwako kwasababu shetani atakuwa na haki ya kuendelea kuwa kwako kwasababu una vitu vyake (dhambi). Tubu dhambi kwa kumaanisha kuziacha, na uziache, na uishi maisha matakatifu ndipo utakuwa na haki ya kufurahia haki zote zilizopatikana kwa kuja na kufa kwa Yesu. Katika **Matendo 19:15,16**, kuna watu ambao walikuwa hawajaokoka wakajaribu kukemea pepo, wapakata madhara. Imelandikwa;

¹⁵ Lakini pepo mchafu akawajibu, “Yesu namfahamu na Paulo pia namfahamu; lakini ninyi ni nani?” ¹⁶ Yule mtu aliyekuwa na pepo mchafu akawarukia akawashambulia vikali, wakatoka ndani ya ile nyumba mbio wakiwa uchi na wenye majeraha.

YESU YU MALAKONI, ANAKUJA KUCHUKUA KANISA

Hizi ni siku za mwisho, Yesu anakuja, yu karibu malangoni, maovu yameongezeka duniani kuliko hata ilivyokuwa kipindi cha sodoma na gomora. Uchafu umezidi duniani, umeingia hata katika nyumba za ibada, wengine badala ya kuhubiri Yesu na nguvu zake wamehamishia kuhubiri vitu vilivyotengenezwa kwa mikono ya wanadamu kama mafuta, maji, chumvi, keki n.k huku wakilaghai watu kwa kupitia Neno la Mungu. Hukumu juu yao itakuwa kubwa kuliko hata hao wanaowapoteza kwasababu wanaujua ukweli lakini hawataki kuufuata.

1Timotheo 4:1 Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengi watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani.

Mungu hajibembelezi kwako, amekupa uhuru uchague kuokoka au ukatae kuokoka, uchaguzi wowote utakaoufanya ndio utakaoakisi hatima ya maisha yako ya sasa na ya baadaye. Usipookoka haumkomoi Mungu au mtu yeyote, yeye ataendelea kubaki Mungu, hapungui kitu.

Kumbukumbu 30:19, imeandikwa, *Nazishuhudia mbingu nan chi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbela yako uzima na mauti, Baraka na laana; basi chagua uzima ili uwe hai wewe na uzao wako.*

Njia yako ya kuokoka ni kwa kumwamini Yesu utu, hakuna njia nyingine. **Yohana 14:6-7**, Yesu akawaambia, Mimi ndimi njia, na kweli na uzima, mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.

Ufunuo 1:7 Tazama yuaja na mawingu na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma, na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam, AMina.

Ufunuo 22:11-12 Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu, na mwenye uchafu azidi kuwa mchafu na mwenye haki azidi kufanya haki na mtakatifu azidi kutakaswa. **Tazama naja upesi na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu sawasawa na matendo yake.**

Ufunuo 21:8 Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katila lile ziwa liwakalo moto na kiberiti.

Yohana 1:12-13 Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina lake; waliozaliwa si kwa damu wala si kwa mapenzi ya mwili wala si kwa mapenzi ya mtu bali kwa Mungu.

Mungu anakupenda sana kuliko tunavyoelewa, na ameweka mbele yako mlango wazi; ukimjia leo atakupokea, hivyo hivyo ulivyo, ukija kwake atakupokea. Pia, hata ukiokoka, kuendelea kuishi maisha matakatifu katika wokovu ni jambo lako binafsi la faida kwako binafsi, kutoendelea haumkomoi Mungu, au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake? **Mathayo 16:26.**

Ufunuo 3:20 Tazama nasimama mlangoni, nabisha, mtu akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango, nitaingia kwake name nitakula pamoja naye nayeye pamoja name.

KUMBUKA: *Kama umeamua kuokoka, nimeandika mfano wa aina ya sala hii unayoweza kusali popote, hata ukiwa chumbani kako peke yako, na kama utamaanisha toka moyoni, Mungu atakupokea na atakuwa jibu la maisha yako. Sali sala hii;*

Eeeh Bwana Yesu, nakuja kwako kwasababu ya kafara la Damu yako, ninatubu dhambi zangu zote (taja unazozijua) ninazo zijua hata zile nisizozijua, ninatubu na kuamua kuziacha, nisafishe dhambi zangu, nisaidie nisikutende dhambi, futa jina langu katika kitabu cha hukumu, andika jina langu katika kitabu cha uzima, kuanzia leo mimi ni mali yako Yesu, kwa Jina lako takatifu, **Amina!**

**Namshukuru Mungu kwasababu nimenawa mikono juu yako
Mungu akubariki!**
